**RIPOTI YA KAMATI YA FEDHA, BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**
**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 110 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, toleo la 2012, ikiwa na majukumu yafuatayo:

(a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.
(b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadiri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.
(c) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.
(d) Kuchunguza na kufatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.
(e) Kuchambuwa mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.
(f) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.
(g) Kuchambuwa ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufatilia utekelezaji wa ahadi hizo.
(h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imepangiwa kusimamia Wizara zifuatazo:

- Wizara ya Kilimo na Maliasili.
- Wizara ya Fedha
- Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

## 1.1 MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilikuwa ina Wajumbe saba na Makatibu wawili, Aidha, baada ya kifo cha Mhe. Salmin Awadh Salmin ambae alikuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Kamati hiyo sasa ina Wajumbe sita na Makatibu wawili kama ifuatavyo:.

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hija Hassan Hija | Makamo Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Asha Abdu Haji | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Hamad Masoud Hamad | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Raya Suleiman Hamad | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| 8. | Ndg. Haji Khatib Haji | Katibu |

## 1.2 UTARATIBU WA KAZI

Kwa mujibu wa Kanuni ya 108 (8), Kamati ilifanya kazi zake kwa utaratibu wa kupokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya Wizara, kukagua baadhi ya maeneo ili kuona hatua za utekelezaji zilizofikiwa na kufuatilia utekelezaji wa Maagizo ya

Kamati. Kwa mwaka huu wa fedha 2014/2015, Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita, kati ya Unguja, Pemba na Tanzania Bara kama ifuatavyo:

- KuanziaTarehe 10 /07/2014 hadi tarehe 23/7/2014 Unguja.

- Tarehe 8/12/2014 hadi tarehe 12/12/2014, Unguja.
- Tarehe 15/12/2014 hadi tarehe 19/12/2014 Tanzania Bara na Unguja.
- Tarehe 2/2/2015 hadi tarehe 6/2/2015 Pemba
- Tarehe 9/2/2015 hadi tarehe 13/2/2015 Unguja.
-

Hata hivyo, kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Kamati ilifanya kazi kwa muda wa wiki mbali Unguja, kuanzia tarehe 27/4/2014 hadi tarehe 3/5/2014. Lengo la kazi hiyo ni kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya taasisi za Serikali katika kipindi cha Julai, 2013-Machi 2014, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

## SEHEMU YA PILI

## WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

### 1.3 MUUNDO WA WIZARA

Wizara ya Kilimo na Maliasili imeundwa na Idara sita (6) na Taasisi moja, Chuo cha kilimo cha Kizimbani na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:

i. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
iii. Idara ya Kilimo
iv. Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka
v. Idara ya Umwagiliaji maji
vi. Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe
vii. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo
viii. Chuo cha Kilimo Kizimbani
ix. Ofisi Kuu ya Kilimo na Maliasili Pemba

### 1.4 MAPATO NA MATUMIZI

Kamati iliarifiwa kuwa katika kipindi cha miezi mitano (Julai - Novemba, 2014), Wizara ya Kilimo na Maliasili iliweza kukusanya mapato ya jumla ya Tsh. 482,014,250 kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Makusanyo hayo ni sawa na asilimia 57 ya lengo lililowekwa la kukusanya jumla ya Tsh. 845,000,000.

Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara ya Kilimo na Maliasili iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 13,758,000,000 ( Tsh. 13,331,000,000 kwa kazi za kawaida na Tsh 427,000,000 ni ruzuku kwa Chuo cha Kilimo, Kizimbani). Kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, 2014 Wizara ilipata jumla ya Tsh. 5,257,9222,338 kwa kazi za kawaida na Chuo cha Kilimo, Kizmbani kilipatiwa Tsh 81,260,000. Fedha zote hizo ni sawa na asilimia 38.22 ya fedha zote zilizotengwa.

Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo Wizara ilitengewa jumla ya Tsh 1,500,000,000 kutoka Serikalini na Tsh 8,339,479,400 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, 2014, Wizara ilipata jumla ya Tsh 227,000,000 sawa na asilimia 15

kutoka Serikalini na Tsh 273,661,387,88 sawa na asilimia 3.3 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

### 1.5 IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Majukumu ya Idara hii ni kusimamia na kuratibu Sera, Sheria, Mikakati, Mipango ya Maendeleo na Utafiti, Idara pia inaratibu mashirikiano ya Wizara na taasisi za ndani na nje ya nchi wakiwemo Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi.

### 1.6 MRADI WA UJENZI WA KITUO CHA MAFUNZO YA USARIFU WA MAZAO (KIZIMBANI)

Mradi wa uanzishwaji wa Kituo cha Mafunzo ya Usarifu wa Mazao ulianza mwaka 2008 ukiwa na thamani ya Dola za Kimarekani 2,300,000 ambazo ni ufadhili kutoka Serikali ya Korea ya Kusini kupitia Shirika la Mashirikiano ya Kimataifa la nchi hiyo (KOICA). Mradi ulijumuisha sehemu kuu tatu ambazo ni Ujenzi wa Kituo cha Usarifu wa Mazao, Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa mradi nchini Korea pamoja na kutoa mafunzo ya vitendo kwa wafanyakazi wa mradi katika kituo hapo Kizimbani, Kuingiza/Kuleta vifaa na mashine za kusarifia, mafunzo pamoja na vifaa vya maabara ya vyakula.

### 1.7 Kazi za Ujenzi

Kazi ya ujenzi ilikuwa ikitekelezwa na kampuni ya KOB iliosajiliwa Kenya ambayo wamiliki wake ni wakorea. Wakati msimamizi mkuu wa ujenzi huo aliajiriwa na KOICA Dar-es-salaam ambae ni Mtanzania. Pia kulikuweko na wasimamizi (site supervisors) walioajiriwa na KOICA kwa vipindi tafauti.

Kamati ilijuilishwa kuwa mkandarasi wa ujenzi huo aliondoka na KOICA waliiambia Wizara kuwa wasingeweza tena kuendelea na ujenzi huo kwa sababu muda wa utekelezaji wake kwa mujibu wa taratibu zao umeshapita. Hata hivyo, waliahidi kuleta wataalamu kwa ajili ya ufungaji wa vifaa na mashine mara ujenzi utakapokamilika pamoja na kubadilisha mashine na vifaa vitakavoonekana vimeharibika.

### 1.8 Kazi zilizokwishatekelezwa hadi hivi sasa

- Kazi ya Ujenzi wa Kituo cha Usarifu wa Mazao imetekelezwa kwa takriban asilimia 80%. Ujenzi huu ulikuwa ukitekelezwa na kusimamiwa na KOICA kupitia kandarasi walioajiriwa na Shirika hilo.
- Mafunzo kwa wafanyakazi wa mradi yametolewa ambapo jumla ya wafanyakazi watano walishiriki mafunzo hayo huko nchini Korea.
- Mashine na vifaa vyote muhimu vilivyohitajika kituoni hapo tayari vimeingizwa nchini na kupokelewa na Wizara.

### 1.9 CHANGAMOTO

1. Kamati ilisikitishwa kuona hali ya kusuasua kwa kazi ya kukamilisha ujenzi wa kituo hicho ambapo jumla ya Tsh. 361,880,000 zinahitajika kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la kituo hicho.
2. Ufungaji wa Mashine na vifaa vya kusarifia, vifaa vya mafunzo pamoja na vifaa vya maabara haukufanyika kutokana na kutokamilika kwa kazi ya ujenzi.
3. Mafunzo ya wafanyakazi kwa vitendo hayakufanyika kwa vile ujenzi haujakamilika.
4. Kamati ilishuhudia kuwepo kwa mashine na vifaa mbali mbali vilivyopo katika ghala la Wizara, Bandarini, Malindi ambavyo viliingizwa nchini muda mrefu sasa (tangu 2010) vikisubiri kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho ambapo ilielezwa kuwa

baadhi ya vifaa hivyo zikiwemo kemikali (reagents) za maabara vimeanza kuharibika.

5. Kazi mbali mbali za ujenzi zinaonekana bado zimebakia zikiwemo, Utiaji wa rangi nje na ndani, Kuweka sakafu katika sehemu zifuatazo; sehemu za kusarifu mazao, stoo,workshop na maabara, Kuweka dari katika sehemu zote za jengo, Kuweka viyoyozi (AC), feni na bulb maeneo yote ya jengo, Kujenga mnara wa tangi la maji ( tank lita 15,000), Kujenga mtambo wa kusarifu maji machafu, Kumalizia fiting ya maji katika shimo la maji (lita 90,000), Kujenga mapokezi ya maji ya mvua, bustani pamoja na maegesho ya gari.

## 2.0 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kamati inaitaka Wizara na Serikali kwa ujumla kutoa kipaumbele katika kulikamilisha jengo la kituo cha usarifu wa mazao, Kizimbani hasa ikizingatiwa kuwa ujenzi wa kituo hicho umashafikia hatua kubwa na vifaa kwa ajili ya kituo hicho vimeshaingizwa nchini muda mrefu vikiwa vimekaa tu bila ya matumizi na vyengine vimeanza kuharibika.

## 2.1 PROGRAMU YA UIMARISHAJI MIUNDOMBINU YA MASOKO (MIVARF)

Kamati iliifuatilia Progamu ya **(MIVARF**) na kuelezwa kuwa ni Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji wa Thamani mazao na Huduma za Fedha Vijijini. Programu hii inayotekelezwa Tanzania nzima ( T/Bara na Zanzibar) kwa mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika,(AIDB) Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo, (IFAD) Mradi huu una vipengele vitatu(3) ambavyo ni :-

a. **Uimarishaji Miundombinu na Mifumo ya Masoko:** Kinahusisha Uendelezaji Miundombinu, Kuongeza thamani mazao na kuongeza uwezo wa wazalishaji na kuwaunganisha na masoko.
b. **Huduma za kifedha vijijini:** Kinahusisha Uendelezaji wa asasi ndogo ndogo za kifedha na uendelezaji mfumo wa kifedha vijijini.
c. **Uratibu:** Kinahusisha kuratibu utekelezaji wa Progarmu kitaif**a.**

Mnamo mwezi wa Febuari, 2015, Kamati ilipata nafasi ya kukagua kazi za ujenzi wa barabara mbalimbali zinazojengwa kwa kiwango cha kifusi Unguja na Pemba kupitia Mradi huu wa MIVARF pamoja na kuonana na wajenzi wa barabara hizo (H Young kwa Pemba na Checo Tech Company kwa Unguja). Barabara zilizotembelewa na Kamati kwa upande wa Pemba ni Mchangamdogo - Mzambarauni yenye urefu wa kilomita 6.1 na Nkanjuni - Kivumoni yenye urefu wa kilomita 3.5. Aidha, kwa Unguja, Kamati ilikagua kazi ya ujenzi wa barabara ya Kibele - Cheju. Pamoja na kuwepo kwa changamoto kadhaa, kwa ujumla Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa kazi za ujenzi wa barabara hizo.

## 2.2 CHANGAMOTO

1. Kusambaa kwa vumbi linalotokana na barabara hizo kunaonekana kuhatarasha afya za wananchi wanaoishi katika maeneo ya karibu na barabara hizo pamoja na kuchafua mazingira na haiba ya maeneo hayo.

2. Baadhi ya wananchi huchukua mchanga katika maeneo ya ujenzi wa barabara hizo.

3. Mifugo (ng'ombe nk) huachiwa na kupita katika barabara hizo zinazoendelea kujengwa na hivyo huharibu na kurudisha nyuma kazi za ujenzi wa barabara hizo.

## 2.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ili kuona umuhimu wa kuziimarisha zaidi barabara hizo zinazojengwa kwa ngazi ya kifusi kupitia Mradi wa MIVARF kwa ajili ya kuwaepusha wananchi wanaoishi karibu na barabara hizo kutokana na athari ya vumbi kwa afya zao pamoja na kuzifanya barabara hizo ziwe imara zaidi.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo na Maliasili kuwa makini katika ujenzi wa barabara zinazojengwa kupitia mradi wa MIVARF kwani Wizara hiyo ndio msimamizi mkuu wa ujenzi.

3. Wizara ishirikiane na mamlaka zinazohusika wakiwemo masheha ili kuhakikisha kuwa vitendo vya wizi wa vifaa vya ujenzi pamoja uharibifu wa barabara hizo vinadhibitiwa ipasavyo.

## 2.4 MTAMBO WA KUZALISHA MAFUTA YA ALIZETI

Katika kazi zake za kawaida, mwezi wa Disemba, 2014, Kamati ilipata nafasi ya kukagua mtambo wa kuzalisha mafuta ya alizeti uliopo Bambi. Kamati iliarifiwa kuwa mashine hiyo yenye uwezo wa kukamua tani sita na nusu kwa siku (6.5) ilinunuliwa Tanzania Bara kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa gharama ya Tshs. 25,000,000.00.

## 2.5 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara iharakishe mpango wake wa kununua mtambo mwengine wa kukamulia alizeti kwa ajili ya wakulima wa Pemba.

2. Wizara inapaswa kuongeza kasi ya kuwahamasisha wakulima wengi zaidi kupanda zao la alizeti kwa vile bidhaa zinazotokana na zao hilo (ikiwemo mafuta) zinaonekana kuwa na soko kubwa hapa nchini.

## 2.6 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Idara hii ina jukumu la kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala katika Wizara, ikiwa ni pamoja na masuala ya ajira, mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu.

## 2.7 CHANGAMOTO

Kuchelewa kujazwa kwa nafasi za kazi zilizoachwa wazi na wafanyakazi waliofariki na waliostaafu limeendelea kuwa ni tatizo linalochangia upungufu wa wafanyakazi wa kada mbali mbali katika Wizara na taasisi zake.

## 2.8 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Katika kutatua tatizo la uhaba wa wafanyakazi Wizara ya Kilimo na Maliasili pamoja na Wizara inayohusika na ajira zinapaswa kutilia mkazo suala la uajiri wa wafanyakazi hususan wenye sifa mahsusi wakiwemo mabwana na mabibi shamba, mafundi na madereva wa matrekta, walinzi na wengineo ili kujaza nafasi zilizopo na kuwapunguzia mzigo mzito wa kazi wafanyakazi wachache waliopo sasa.

2. Wizara iandae mipango ya muda mrefu kwa ajili ya mafunzo ya wafanyakazi wake wakiwemo wafanyakazi wa kada ya utafiti wa kilimo.

**2.9 IDARA YA KILIMO**

Idara hii ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, upatikanaji na usambazaji wa huduma za pembejeo na zana za kilimo kwa wakulima, uhifadhi na ukaguzi wa mazao na kutoa mafunzo kwa wakulima.

**3.0 CHANGAMOTO**

1. Kuchelewa kwa wakulima kulipia gharama za kulimiwa mashamba yao kwa wakati hususan kwa msimu huu. Kamati imebaini kuwa eneo kubwa la mpunga unaotegemea mvua katika bonde la Cheju lilikuwa bado halikulimwa kwa wakati huo kutokana na tatizo hilo.
2. Uhaba na uchelewaji wa fedha katika Wizara husika. Kutokana na uhaba huo wa fedha pamoja na uchelewaji wake kutoka Wizara ya Fedha nao pia huchangia kuchelewa kwa matayarisho ya mashamba ya mpunga.
3. Upungufu wa vitendea kazi ikiwemo majembe ya kuburugia (ya matrekta). Aidha, vitendea kazi vilivyopo ni vichakavu na havihimili kufanyia kazi. kwa mfano, baadhi ya matrekta yaliopo ni ya zamani na hayawezi kuhimili kazi zilizopo.
4. Udhaifu wa matrekta mapya ambapo Kamati ilielezwa kwamba matrekta yalionunuliwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili hivi karibuni ni dhaifu na hayastahamili kazi nzito wa kazi kwa vile baadhi ya maeneo yana ardhi ngumu jambo ambalo limeyafanya matrekta hayo kuharibika na kufanyiwa mategenezo siku hadi siku.
5. Uhaba wa mafundi na madereva wa matrekta umeendelea kuwa ni kikwazo kikubwa kutokana na kustaafu kwa wafanyakazi wakongwe na kutojazwa kwa nafasi walizoziacha na kutoajiriwa kwa wafanyakazi wapya.

**3.1 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara kufanya utafiti wa kina juu ya vifaa vilivyomo katika matrekta kabla ya kununua matrekta hayo ili matrekta yanayonunuliwa yaweze kumudu hali halisi ya ardhi katika mashamba mbali mbali.

2. Wizara inapaswa kuwashirikisha wataalamu wake kikamilifu katika hatua zote muhimu za ununuzi wa vifaa vya kilimo ili kuepukana na ununuzi wa vifaa visivyokidhi mahitaji halisi.

3. Kamati inaishauri Wizara kuengeza jitihada za kutoa elimu kwa wakulima hususan wa kilimo cha mpunga wa kutegemea mvua, ili waweze kubadilika na kufanya matayarisho ya kilimo cha mpunga mapema kulingana na mabadiliko ya miongo na hali ya hewa duniani hivi sasa.

4. Kwa kuwa matayarisho ya kilimo cha mpunga hufanywa kwa wakati maalum ni vyema Wizara na Serikali kujipanga vizuri zaidi kwa kuhakikisha upatikanaji wa fedha wa uhakika na wa wakati ili kuwaondoshea wakulima usumbufu unaotokana na athari ya kuchelewa kwa matayarisho ya mapema ya kilimo hicho.

## 3.2 IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI

Idara hii ina majukumu ya kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji nchini pamoja na kutoa taaluma za kiufundi juu ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji. Idara pia ina jukumu la kushajiisha na kusimamia jumuiya za wakulima kwenye mabonde ya umwagiliaji sambamba na kutoa elimu ya utaalamu ya teknolojia ya kilimo cha umwagiliaji maji. Kamati ilipata nafasi ya kutembelea mabonde mbali mbali ya umwagiliaji maji pamoja na vituo vya umwagiliaji maji katika mabonde hayo. Miongoni mwa mabonde hayo ni Kibokwa, na Cheju kwa Unguja na Makombeni kwa Pemba.

## 3.3 Bonde la Kibokwa

Kamati ilipata nafasi ya kutembelea kituo cha umwagiliaji maji katika bonde la Mpunga la Kibokwa pamoja na kuzungumza na Kamati ya wakulima wa bonde hilo mnamo mwezi wa Disemba, 2014.

## 3.4 CHANGAMOTO

1. Wakulima wanakabiliwa na tatizo la mzigo wa gharama za umeme ambapo kila mkulima hutakiwa kuchangia Tsh 50,000 kwa mwezi kwa ajili ya kugharamia huduma za umeme kwa kilimo cha umwagiliaji maji.
2. Kituo cha umwagiliaji cha Kibokwa ni kibovu na kinahitaji kufanyiwa ukarabati.
3. Tatizo la kuwepo kwa mitaro ya zamani.
4. Kituo kina uhaba wa walinzi hususan katika sehemu zilizopo mashine za kusukumia maji.

## 3.5 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kwa kuwa changamoto kadhaa zinatarajiwa kuondoka baada ya kuanza kwa utekelezaji wa mpango mkuu wa umwagiliaji maji, kuna haja kwa Serikali hivi sasa kuiingilia kati changamoto sugu ya gharama za umeme wa kilimo cha umwagiliaji maji ili kutoa unafuu kwa wakulima wa kilimo hicho ambao wamekuwa na kilio hicho kwa muda mrefu sasa.

## 3.6 Bonde la Makombeni (Pemba)

Kamati imeridhishwa kuona kuwa Idara kwa kushirikiana na wakulima wa bonde la Makombeni wameanza kufanikisha kazi ya kuweka sawa (levelling) sehemu ya bonde hilo yenye ukubwa wa hekta sita (6) na shughuli za kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji katika sehemu hiyo iliyowekwa sawa zimeanza kufanyika kwa ufanisi mkubwa kwa vile mpunga uliooteshwa ulikuwa umestawi vizuri. Aidha, Kamati imefarajika kuona kuwa Idara kwa kushirikiana na wakulima wa bonde hilo wana mpango wa kuliweka sawa eneo jengine lililobakia katika bonde hilo ili hatimae bonde hilo lote lenye ukubwa hekta 12 liwe limekamilika kwa ajili ya kilimo cha umwaguliaji maji.

## 3.7 CHANGAMOTO

1. Mtaro kwa ajili ya kukidhi umwagiliaji wa bonde lote unahitajika kwa vile uliopo sasa hauwezi kukidhi haja hiyo kikamilifu.
2. Kuna haja ya kuchimbwa kisima kipya kwa kuwa kisima kilichopo sasa hakina uwezo wa kumwagilia maji bonde lote la Makombeni.
3. Kuna baadhi ya sehemu katika bonde hilo bado zinahitaji kazi ya kuwekwa sawa (levelling).

## 3.8 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kamati inaitaka Wizara kuharakisha mpango wake wa kuandaa michoro (design) kwa ajili ya kazi ya uwekaji sawa wa eneo lililobakia la bonde la Makombeni ili hatimae wakulima wote wa bonde hilo waweze kufaidika na kilimo cha umwagiliaji maji.

**3.9 IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE**

Idara hii ina jukumu la kuratibu kazi za uhakika wa chakula na lishe ikiwa ni pamoja na kufuatilia, kutathmini, na kutoa taarifa juu ya hali ya uhakika wa chakula na lishe na tahadhari ya mapema juu ya matukio yanayohusiana na hali ya uhakika wa chakula na lishe hapa nchini. Idara pia ina jukumu la kusimamia na kuendesha Hifadhi ya Chakula ya Zanzibar (Zanzibar Food Reserve).

**4.0 CHANGAMOTO**

Katika ripoti ya utekelezaji wa kazi za Wizara kwa kipindi cha miezi mitano ( Julai hadi Novemba, 2014) ilielezwa kuwa kazi ya kukarabati ghala la Hifadhi ya Taifa ya Chakula imechelewa kufanyika kwa kuwa hadi wakati wa kuwasilishwa kwa ripoti hiyo mbele ya Kamati (mwezi wa Disemba, 2014), Idara ilikuwa haijatiliwa fedha zilizopangwa kwa ajili ya kazi hiyo. Aidha, Kamati mnamo mwezi wa Febuari, 2015 ilikagua moja kati ya ghala za Wizara hapo bandarini, Malindi na kukuta kuwa kazi ya ukarabati wa ghala bado haijaanza.

Aidha, Kamati imegundua kuwa hata katika miaka ya fedha ya nyuma ukiwemo mwaka jana (2013/2014) kazi hii ya ukarabati wa ghala la Hifadhi ya Chakula ilikosa kufanyika kutokana na kutoingiziwa fedha.

**4.1 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

Kwa kuwa ni muda mrefu sasa kazi ya ukarabati wa ghala la Hifadhi ya Chakula, haijafanyika kutokana na kutoingiziwa fedha ipo haja kwa Wizara na Serikali kwa ujumla kuona umuhimu mkubwa wa nchi yetu kuwa na ghala la Hifadhi ya Chakula linalofanyakazi ili kuweza kukidhi mahitaji ya dharura ya chakula hapa nchini.

**4.2 IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA**

Idara ina jukumu la kulinda na kuhifadhi misitu na wanyamapori, kusimamia mashamba ya misitu na mbegu, upatikanaji wa miche bora, kuhamasisha kilimo cha biashara na kuratibu uvunaji wa maliasili zisizorejesheka.

**4.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira zipitie viwango vya ada zinazotozwa kwa kampuni za miradi mikubwa zinazochimba na kuchukua maliasili (kifusi, mchanga, matofali nk) kwa kiasi kikubwa pamoja na kufanya tathmini ya kina ya faida wanayopata wananchi na Idara husika pamoja na athari ya kimazingira katika maeneo yanayochimbwa na kuchukuliwa maliasili hizo.

**4.4 CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI**

Jukumu kubwa la Chuo hiki ni kutoa mafunzo katika fani za kilimo, maliasili na mifugo katika ngazi tofauti. Pamoja na jukumu hilo, Chuo pia kina jukumu la kulisimamia na kulitumia shamba la RAZABA lililopo Bagamoyo, Tanzania Bara.

## 4.5 SHAMBA LA RAZABA, MAKURUNGE - BAGAMOYO.

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilipokea taarifa ya utekelezaji kuhusu shamba la RAZABA ( Ranch ya Zanzibar Bagamoyo) pamoja na kutembelea shamba hilo la Wizara ya Kilimo na Maliasili lililopo Bagamoyo mnamo tarehe 17/12/2014.

Kamati ilipewa taarifa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha shamba la Mifugo ya Ngo'mbe wa nyama huko Makurunge Wilaya ya Bagamoyo Tanzania Bara ili kukidhi mahitajio yake ya kitoweo nchini. Uamuzi huo ulitokana na uhaba wa ardhi Visiwani humu na kulazimika kuomba ardhi Tanzania Bara kwa ajili ya kufunga idadi kubwa ya ngo'mbe itakayokidhi haja. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikubali ombi hilo na kupatiwa shamba hilo lililokuwa na ukubwa wa hekta 28,200 ambalo maarufu lilijulikana kwa jina la RAZABA (Ranch ya Zanzibar Bagamoyo) ambayo ilianzishwa rasmi Oktoba 1976.

Shamba hilo liliendelea na harakati zake za ufugaji hadi mwaka 1994, Serikali ilipolazimika kusitisha kazi hizo kutokana sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na uhaba wa fedha na mabadiliko ya Sera za kiuchumi zilizopelekea kufungua milango ya biashara kwa sekta binafsi na kuiachia biashara hiyo kuendelezwa na sekta binafsi.

Mwaka 2007, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliridhiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuligawa shamba hilo sehemu mbili zenye ukubwa wa hekta 22,000 na 6200 kila moja ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sasa imebakiwa na hekta 6200 na hekta 22,000 zimechukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muunagano wa Tanzania kwa maendeleo mengine chini ya uwekezaji wa ubia na kampuni ya kigeni.

Baada ya mabadiliko hayo ya mgawanyo wa shamba hilo kila upande umetakiwa uwe na hati miliki, mchakato ambao unaendelea ambapo kwa upande wa Zanzibar ili kukidhi vigezo vya kisheria vya kupata hati ya shamba hilo, imelazimika kukabidhiwa Chuo cha Kilimo, Kizimbani ambacho ni Taasisi yenye uwezo wa kumilikishwa shamba kwa mujibu wa Sheria Namba 5 ya 2007 iliyokianzisha Chuo hicho.

Mchakato wa ufuatiliaji wa hati miliki ya shamba hilo unaendelea kwa kufanya mawasiliano ya karibu na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Taasisi mbili ndizo zenye kuhusika na utoaji wa hati miliki na mipango matumizi ya eneo hilo.

Hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kama zifuatazo:-

i. Kuomba hati miliki ya shamba hilo.
ii. Kuweka usimamizi makini na kuimarisha ulinzi. ( Kuweka mabango manane katika pande zote za mipaka ya shamba la RAZABA, Pikipiki moja imeshanunuliwa na Bunduki 5 zimelipiwa kodi).
iii. Kuandaa mpango wa matumizi wa eneo hilo.

## 4.6 CHANGAMOTO

1. Kamati imegundua kuwa baadhi ya maeneo ya shamba hilo yamevamiwa na wananchi wa Bagamoyo kwa ujenzi, malishio ya wanyama na kilimo.

2. Licha ya juhudi za Wizara za kuomba hatimiliki ya eneo hilo, hadi Kamati ilipolitembelea shamba hilo (tarehe 17/12/2014), hatimiliki ya shamba hilo ilikuwa bado haijipatikana.
3. Eneo hilo tayari lipo katika mpango kazi wa mradi wa maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wake nayo ina mpango wake wa matumizi wa eneo hilo.

**4.7 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujumla kukaa pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kupata njia muafaka ya kuzitatua changamoto za shamba la RAZABA ikiwa ni pamoja na kufanikisha kupatikana kwa hatimiliki ya shamba hilo.
2. Kwa kuwa shamba hilo la RAZABA lina maeneo tofauti likiwemo eneo la ufukweni kuna haja kwa Serikali kuzingatia kwa makini matumizi ya shamba hilo ili matumizi hayo yalingane na maumbile halisi ya eneo hilo na hatimae kuweza kutoa tija kubwa zaidi kwa Serikali na kwa wananchi wa Zanzibar kwa ujumla.

**4.8 TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO, KIZIMBANI**

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo(Kizimbani) ambayo ilianzishwa mwaka 1933 ambapo ilikuwa ikijulikana kama ni Kituo cha Utafiti wa Kilimo, imeanzishwa rasmi kwa Sheria No. 8 ya 2012.

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ina jukumu kubwa la kubuni, kupanga na kutekeleza kazi za Utafiti katika sekta za Kilimo na Maliasili na kutoa matokeo yake kwa walengwa wakiwemo wakulima, wanafunzi, na wadau wengine. Taasisi inajumuisha vituo vyote vya utafiti vilivyo ndani ya Sekta ya Kilimo na Maliasili. Katika mwaka huu wa fedha wa 2014/2015, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea na kupokea taarifa ya utekelezaji wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Kizimbani) mnamo tarehe 11/12/2014.

**4.9 CHANGAMOTO**

1. Uhaba wa bajeti ya Serikali katika kutekeleza kazi za Utafiti (mwaka jana 2013/2014 bajeti ilikuwa milioni 140, ambapo zilipatikana asilimia 10 tu na mwaka huu 2014/2015, bajeti ni milioni 300 ambapo hadi Kamati ilipokuwa katika Taasisi hiyo (tarehe 11/12/2014 fedha zilizopatikana ni milioni 20 sawa na asilimia 7 tu ya makadirio.
2. Usafiri kwa wafanyakazi na watafiti ( Taasisi ina gari ndogo za pick up tu ambazo mbili ni chakavu sana. Gari hizo ni kwa ajili ya kazi zote za Taasisi ikiwemo kuchukua na kurejesha wafanyakazi katika maeneo yao).

3. Uchache wa wataalamu ambapo wengi wao wanastaafu katika miaka mitatu mpaka mitano ijayo.

4. Kukosekana kwa Baraza la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo pamoja na Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Taasisi hiyo. Kamati imegundua kuwa tangu mwaka 2012 ilipopitishwa Sheria hiyo Taasisi hiyo imekuwa ikifanyakazi bila ya kuwa na Kanuni wala Baraza. kutokana na hali hiyo Taasisi hiyo imekuwa ikifanya kazi zake katika mazingira magumu.

## 5.0 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara kukamilisha Kanuni za Sheria ya Utafiti wa Kilimo ili Taasisi hiyo ya Utafiti wa Kilimo kuweza kufanya kazi zake kwa mujibu wa taratibu za Sheria.
2. Kamati inaisisitiza Wizara na Serikali kwa ujumla kutoa kipaumbele maalum katika kuingiza fedha kwa ajili ya utafiti wa kilimo kwa vile fedha zinazoingizwa hivi sasa ni kidogo sana na hivyo kuzorotesha kazi za utafiti ambazo hutegemewa sana katika maendeleo ya kilimo.

## 5.1 KITUO CHA UTAFITI WA KILIMO CHA MATANGATUANI (PEMBA)

Kituo hiki ndio Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo kwa upande wa Pemba, Kituo kina eneo lenye ukubwa wa eka arobaini (40) ambazo ndani yake kuna mazao ya kudumu, mazao ya msimu, maeneo ya wazi na mabonde. Kituo kinaendesha tafiti mbali mbali za mazao ya biashara (karafuu), mazao ya nafaka (mpunga, mahindi), mazao ya jamii ya kunde (kunde), mazao ya mboga (tungule, mchicha, bilingani, bamia na nyanya chungu), mazao ya mizizi (viazi, muhogo) na tafiti za migomba.

Miongoni mwa tafiti ambazo Kamati ilizikuta zikiendelea wakati ilipotembelea kituo hicho mwezi wa Febuari, 2015 ni utafiti wa uzalishaji wa miche ya mikarafuu kwa kutumia aina tofauti za udongo na viwango tofauti vya umwagiliaji maji.

## 5.2 CHANGAMOTO

1. Uhaba mkubwa wa fedha za kuendeshea tafiti. Kazi za utafiti zinazofanywa zinatokana na fedha kidogo za maendeleo zilizopatikana, hali hiyo pia inapelekea kukosekana kwa uhakika wa hatma ya utafiti muhimu wa miche ya mikarafuu unaoaendelea kituoni hapo ambao unahitaji Tsh.15 millioni hadi kukamilika kwake.

2. Upungufu wa wahudumu wa shamba ambapo kwa sasa kituo kina wahudumu wa shamba sita (6) na mahitaji ni angalau wahudumu 15 ili kusaidia katika kazi za umwagiliaji na upaliliaji katika tafiti mbali mnali.

3. Uhaba wa watafiti ambapo kwa sasa kituo kina watafiti wenye shahada ya pili (Master degree) wawili na wenye shahada ya kwanza (BSc) mmoja ambapo mahitaji halisi ni PhD wawili, MSc watatu, BSc watano, Diploma kumi, na Cheti (Certificate) watano. Mahitaji hayo ni katika fani tofauti.
4. Kutokuwa na jengo la ofisi ambapo kwa sasa ofisi ya kituo ipo katika hatua za matengenezo na jengo la maabara linatumika kama ofisi.

5. Kutokuwepo kwa jengo bora la maabara na vifa vyake.

6. Uhaba wa vyombo vya usafiri ambapo kwa sasa kituo kina gari moja kwa Pemba.

## 5.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kamati inaitaka Wizara kufanya kila jitihada ili kuwezesha upatikanaiji wa fedha (Tsh millioni 15) zinazohitajika kwa ajili ya kukamilisha utafiti wa miche ya mikarafuu katika kituo cha Utafiti cha Matangatuani (Pemba) kutokana na umuhimu mkubwa wa utafiti huo katika uchumi wa nchi yetu.

## 5.4 OFISI KUU PEMBA

Ofisi hii ya Pemba ni kiunganishi katika kuhakikisha majukumu, malengo na kazi zote za Wizara kwa Pemba zinatekelezwa kama zilivyoainishwa katika Idara na Taasisi za Wizara.

## 5.5 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kwa kuwa eneo la Ole lina vyanzo vingi vya maji (maziwa) Wizara ifanye juhudi ya kuandika miradi (Project Write Up) na kutafuta wafadhili kwa ajili ya kilimo cha mboga mboga katika eneo hilo na hivyo itasaidia sana kuondoa upungufu wa mboga mboga na kuondokana na usumbufu wa kuagiza mboga mboga kutoka Tanzania Bara.

**SEHEMU YA TATU**

**WIZARA YA FEDHA**

Wizara ya Fedha inashughulikia kazi za idara saba na taasisi nane zinazojitegemea ambazo ni;

| **Idara** | **Taasisi** |
|---|---|
| 1. Idara ya Bajeti, | 1. Bodi ya Mapato ya Zanzibar |
| (ZRB) | |
| 2. Idara ya Fedha za nje, | 2. Mamlaka ya Mapato |
| Tanzania (TRA) | |
| 3. Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, | 3. Mfuko wa Barabara wa |
| Zanzibar | |
| 4. Idara ya Uhakikimali na Mitaji ya Umma, | 4. Mfuko wa Hifadhi ya |
| Jamii,Zanzibar | |
| 5. Idara ya Uendeshaji na Utumishi, | 5. Shirika la Bima la Zanzibar |
| 6. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, | 6. Mamlaka ya Ukuzaji Vitega |
| Uchumi, | |
| 7. Ofisi kuu ya Pemba | 7. Benki ya Watu wa Zanzibar |
| (PBZ) | |
| | 8. Chuo cha Uongozi wa Fedha, |
| Zanzibar | |

## 5.6 MAPATO NA MATUMIZI

Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara ilipangiwa kukusanya jumala ya Tsh 386.80 bilioni ambapo kwa kipindi cha Julai - Novemba, 2014 iliweza kukusanya Tsh.143.46 bilioni sawa na asilimia 37 ya lengo la mwaka.

Aidha, kwa mapato yasiyokuwa ya kodi,(Non Tax Revenue), jumla ya Tsh. 6.0 bilioni zilitarajiwa kukusanywa katika mwaka 2014/2015 ambapo hadi kufikia mwishoni mwa mmwezi Novemba, 2014, Wizara ilikwishakusanya jumla ya Tsh. 1.06 bilioni sawa na asilimia 18 ya makadirio ya mwaka.

Vili vile, kwa mwaka huu wa fedha, jumla ya Tsh. 306.04 bilioni ikiwemo misaada ya kibajeti ya Tsh. 40 bilioni zilikadiriwa kupatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Taasisi za Kimataifa. Fedha halisi zilizoripotiwa kupatikana hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Novemba, 2014 ni Tsh. 37.21 bilioni.

Aidha, katika kutekeleza majukumu yake ya kawaida kwa kipindi cha miezi mitano (Julai - Novemba) cha mwaka 2014/2015, Wizara ilipatiwa jumla ya Tsh 11.45 bilioni kama ni matumizi ya kazi za kawaida ikiwa ni sawa na asilimia 85 ya makadirio ya Tsh 13.47 billioni ya kipindi hicho. Fedha zilizotumika kwa ajili ya ulipaji mishahara ya wafanyakazi wa Wizara ni Tsh 1.96. Aidha, jumla ya Tsh. 6.98 bilioni zilitolewa kama ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii ni sawa na asilimia 87 ya makadirio ya Tsh 8.0 bilioni ya kipindi cha miezi mitano (Julai -Novemba, 2014)

Kwa upande wa matumizi mengineyo, jumla ya Tsh 2.51 bilioni zilitumika sawa na asilimia 75 ya makadirio ya kipindi hicho (Julai - Novemba, 2014) mbazo ni Tsh. 3.35 bilioni. Vile vile, Wizara ilipangiwa kutekeleza na kuratibu jumla ya Programu tano na Miradi mitatu ya maendeleo. Katika mwaka 2014/2015, Programu na Miradi ya Wizara ilitengewa jumla ya Tsh. 27.20 bilioni kama mchango wa Serikali katika miradi na Programu hizo. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Novemba, 2014, Wizara ilipatiwa jumla ya Tsh. 10.82 bilioni kama ni mchango wa Serikali sawa na asilimia 40 ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Wizara ilitarajia kupokea jumla ya Tsh 13.56 bilioni na kwa kipindi hicho cha Julai - Novemba, 2014, ilitarajia kupokea jumla ya Tsh 6.46. Fedha zilizopokelewa hadi mwishoni mwa mwezi wa Novemba zilifikia Tsh. 6.33 bilioni sawa na asilimia 98 ya makadirio ya miezi mitano na asilimia 47 kwa lengo la mwaka.

**5.7 IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

Idara hii ina jukumu la kuandaa Sera na Mipango inayohusu fedha na kodi na kusimamia utafiti katika sekta ya fedha.

**5.8 MRADI WA HUDUMA ZA JAMII MIJINI (ZANZIBAR URBAN SERVICE PROJECT/ ZUSP)**

Mradi wa Huduma za Jamii Mijini (ZUSP) ni Mradi ambao utekelezaji wake umekuwa ukiulizwa sana na wananchi na baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokana na ukimya wake wa muda mrefu. Mradi huu unakusudia kuimarisha na kuendeleza huduma pamoja na kujenga uwezo wa kitaasisi wa Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji Mikuu ya Chake Chake, Wete na Mkoani.

**5.9 Utekelezaji wa kazi za Mradi hadi Novemba, 2014**

i. **Kazi za ukarabati wa jengo la Manispaa** (kwa makisio ya gharama ya Tsh. 1,230,000,000): Kazi hiyo inaendelea, hata hivyo yamejitokeza matatizo yakiwemo jengo kudidimia, na paa la jengo hilo kutofaa tena. Matatizo yaliyojitokeza yatagharimu fedha za ziada takriban millioni 400, gharama ambazo zimeshatumwa kwa mfadhili na zinafanyiwa kazi.

ii. **Kazi ya Ujenzi wa Mitaro ya maji ya mvua**( (kwa makisio ya gharama ya Tsh 13,280,000,000):Zabuni zimashatangazwa tangu tarehe 14, Novemba, 2014 na zilitarajiwa kufunguliwa tarehe 30, Disemba 2014. Baada ya hapo zitafuata kazi za tathmini za kumpata mjenzi.

iii. **Kazi ya uwekaji taa za barabarani:** (kwa makisio ya gharama ya Tsh. 4,000,000,000):Taratibu za zote za zabuni zimekamilika zikiwemo utoaji wa matangazo, uuzaji wa zabuni, ufunguzi na tathmini. Ripoti ya tathmini imeshakabidhiwa kwa Katibu Mkuu na hatua za mazungumzo zilitarajiwa kufanyika mara baada ya sikukuu ya Krismasi na baadae kusaini mkataba kusaini mkataba na kuanza kazi.

iv. **Kazi za ujenzi wa kufanywa vizimba vya taka**: (Kwa makisio ya gharama ya Tsh. 893,113,690):.Kazi za ujenzi zinaendelea na kampuni ya M/S Zeccon ya Zanzibar. Hapo awali vilipangwa kujengwa vizimba 193 lakini kutokana na kukosekana kwa maeneo vilipunguzwa hadi 80 na hadi sasa jumla ya vizimba vya taka 56 vimekamilika. Kwa sasa hawajapatiwa maeneo mengine. Aidha, kwa ushauri wa Benki ya Dunia ( World Bank), Kampuni ya Zeccon imeongezewa kazi ya kuweka "apron" katika vizimba vilivyojengwa ili kuweka mazingira mazuri kwa waendao kutupa taka na jumla ya vizimba 30 vimeshafanyiwa marekebisho hayo.

v. **Ujenzi wa Miradi midogo midogo ya Mabaraza ya Miji ya Pemba** (kwa makisio ya gharama ya Tsh 3,840,000,000): Taratibu zote zaa Zabuni zimekamilika zikiwemo utoaji wa matangazo, uuzaji wa Zabuni, ufunguzi wa tathmini. Ripoti ya tathmini imeshakabidhiwa kwa Katibu Mkuu na hatua za mazungumzo zilitarajiwa kufanyika baada ya Sikukuu ya Krismasi na baadae kusaini mkataba na kuanza kazi

vi. **Ujenzi wa ukuta wa bahari, Mizingani** (kwa makisio ya gharama ya Tsh.12,280,000,000). Taratibu zote za Zabuni zimekamilika zikiwemo utoaji wa matangazo, uuzaji wa zabuni, ufunguzi na tathmini ameshakabidhiwa Katibu Mkuu kwa hatua za kuipeleka Benki ya Dunia kwa kupata "No Objection"

## 6.0 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kamati inaitaka Wizara kuwa makini katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati kwani kuendelea kutekeleza miradi isiyokwisha kunaigharimu zaidi Serikali kwa kuwa gharama za kutekeleza miradi hiyo inayochukua muda mrefu kukamilika zinaongezeka kadiri inavyochokuua muda mrefu kukamilika kwake.

## 6.1 IDARA YA FEDHA ZA NJE

Idara hii ina jukumu la kutafuta misaada kutoka nje ya nchi na kuratibu mahusiano ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

## 6.2 CHANGAMOTO

Hadi mwezi wa Disemba, 2014 wakati Kamati ilipokuwa inapokea taarifa ya utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, 2014, iliripotiwa kuwa kwa kiasi kikubwa misaada ya kibajeti kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa imesitishwa na wafadhili kutokana na sakata la Akaunti ya "**Tegeta Escrow**" hali ambayo imepelekea mambo mengi hususan ya kiutendaji kukwama.

## 6.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kuna haja kwa Serikali kufanya utafiti wa kina juu ya athari za sakata la 'Tegeta Escrow" kwa Serikali na uchumi wa nchi wa Zanzibar pamoja na kuandaa mikakati madhubuti ya

kukabiliana na masakata makubwa kama hayo yenye athari kubwa kwa uchumi wa nchi yetu.

**6.4 OFISI KUU - PEMBA**

Ofisi kuu ya Wizara ya Fedha, Pemba ndio inayotekeleza kazi zote za Wizara kwa Pemba.

**6.5 CHANGAMOTO**

1. Jengo linalotumiwa na Ofisi ya Wizara ya Fedha, Pemba kwa sasa ni bovu na Kamati imebaini kuwa hata ofisi ya Afisa Mdhamini wa Wizara hiyo ina nyufa zinazohatarisha usalama wa wafanyakazi wa ofisi hiyo.
2. Kutotumika kwa akaunti ya fedha za maendeleo, Pemba iliyowekwa kwa ajili ya kuwekwa fedha za kazi za maendeleo zinazotumika kwa upande wa Pemba.
3. Kukosekana katika Ofisi hiyo kwa baadhi ya kumbukumbu za kikazi zikiwemo za matumizi ya fedha za maendeleo za taasisi mbali mbali za Serikali zilizoko Pemba pamoja na kumbukumbu za wastaafu kutoka Pemba waliopewa kiinua mgongo.
4. Kuwepo kwa mgonngano wa kimuundo baina ya Ofisi ya Wizara ya Fedha, Pemba na Wizara nyengine kwa Pemba ambapo Ofisi hiyo imezigawa sehemu zake na kuziita kuwa Divisheni wakati Wizara nyengine kwa Pemba zimegawa sehemu zao na kuziita kuwa ni Idara.

**6.6 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Wizara ichukue hatua za haraka za kukabiliana na tatizo la ubovu wa jengo linalotumiwa na Wizara kwa Pemba kwa kuwa jengo hilo linahatarisha maisha ya wafanyakazi wa ofisi hiyo.
2. Kuna haja kwa Wizara kuweka mfumo mzuri zaidi wa kuiunganisha Ofisi ya Wizara iliyopo Pemba ili kumbukumbu muhimu za kikazi zikiwemo za matumizi ya fedha za maendeleo za taasisi za Serikali zilizopo Pemba pamoja na kumbukumbu za wastaafu waliopewa kiinua mgongo ziweze kupatikana katika Ofisi hiyo.
3. Wizara ishirikiane na Wizara inayohusika na Utumishi wa Umma ili kuliweka sawa suala la muundo wa Ofisi ya Wizara hiyo, Pemba na kutumia majina stahiki katika sehemu zake (baina ya Idara au Divisheni) kwa mujibu wa taratibu.

**6.7 SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR**

Shirika lina jukumu la kutoa huduma za Bima kwa ujumla. Kamati katika nyakati tofauti, ilitembelea ofisi mbali mbali za Shirika hilo zilizopo Mbeya na Pemba pamoja na kukukutana na Bodi ya Shirika hilo, Mpirani, Unguja.

**6.8 OFISI YA SHIRIKA LA BIMA, MBEYA**

Ofisi hii ya Nyanda za juu Kusini ilianzishwa rasmi mwezi Julai 2009 ikiwa na lengo la kutoa huduma bora kwa eneo lote la kanda ya Nyanda za juu Kusini lenye Mikoa ya Iringa, Ruvuma,Mbeya, Rukwa, Njombe na Katavi. Kwa mwaka wa fedha 2014 Ofisi hii ya Kanda Nyanda za Juu Kusini ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh 1,562,990,000/=. Mapato halisi kwa Januari-Disemba ni Tsh 2,036,107,038/= ikiwa ni ziada ya Tsh 473,117,038/= kwa malengo ya 2014, hii ni sawa na ziada ya 30%.Kwa upande wa matumizi, kwa miezi Tisa ya Januari - December 2014 ofisi ilipangiwa kutumia jumla yaTsh 156,379,956 kwa matumizi ya kawaida.Matumizi hasa ni Tsh 97,303,115.50 Matumizi haya hayajumuishi mishahara ambayo inalipwa Makao Makuu ya Shirika.

Aidha ofisi imetumia Tsh 256,654,023.30 kwa kulipia Ujira kwa mawakala.

### 6.9 CHANGAMOTO

1. Kanda inaendelea kupokea madai mengi pamoja na juhudi kubwa ya kufatilia kwa karibu ajali hizo ili kuepusha kufanyiwa udanganyifu.

2. Biashara inaendelea kukua na hali ya upatikanaji wa mtandao wa Ofisi si wa uhakika, hivyo kusababisha baadhi ya nyakati data kutoingizwa kwa wakati.

3. Baadhi ya makampuni yanaendelea na mbinu chafu za kiushindani ikiwemo kuwarubuni mawakala wa Shirika na kushusha viwango vya malipo tulivyokubaliana kwa pamoja kutumika kwenye soko.

### 7.0 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Shirika la Bima lijiwekee mipango ya muda mrefu kujenga ofisi zao takriban katika kanda zote ili kuliepusha Shirika na gharama kubwa ya kulipia kodi katika majengo mengi linayoyatumia sasa.

### 7.1 OFISI YA SHIRIKA LA BIMA, PEMBA

Kamati ilipewa taarifa kuwa katika kipindi cha Julai - Disemba, 2014 Kituo cha Pemba kilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh 100,240,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali na kimeweza kukusanya jumla ya Tsh 153,229,414 sawa na asilimia 153 ya lengo kwa kipindi hicho.

Kwa upande wa matumizi, katika kipindi cha Julai- Disemba, 2014, Kituo cha Pemba kilipangiwa kutumia Tsh 14,464,938 kwa kazi za kawaida. Matumizi halisi ya miezi hiyo sita (6) ni jumla ya Tsh 11,575,500 sawa na asilimia 80 ya makadirio ya ya matumizi kwa kipindi hicho.

### 7.2 CHANGAMOTO

1. Kutokatiwa Bima kwa baadhi ya vyombo vya Serikali ambapo ni kwenda kinyume na utaratibu wa Sheria za nchi.

2. Baadhi ya wananchi hawataki kukata Bima kwa hiari mpaka vishirikishwe na vyombo vya ulinzi.

3. Ukosefu wa jengo bora kwa shughuli za Ofisi. Ofisi bado haijamiliki jengo lake na maeneo ilipo ofisi hiyo hivi sasa wateja wanapata usumbufu na kupoteza hadhi ya Shirika katika kipindi hiki cha ushindani wa kibiashara.

### 7.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kwa kuwa redio Istiqama na redio Michweni ndizo redio zinazosikilizwa sana na wananchi wengi wa Pemba, Kamati italishauri Shirika la Bima kuzitumia redio hizo kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi wa Pemba juu ya umuhimu wa kukata bima na athari mbali mbali zinazoweza kuwapata wananchi kwa kutokata bima.

2. Shirika la Bima lizidishe mashirikiano na wadau mbali mbali ili kuhakikisha kuwa magari ya taasisi za Serikali pamoja ya vyama vya siasa yanakatiwa Bima kwa mujibu wa Sheria.

3. Kuna haja kwa Shirika kuandaa semina kwa Makatibu Wakuu pamoja na Wakuu wa Idara ili kuwaelimisha juu ya umuhimu wa kukatiwa bima kwa majengo mbali mbali ya Serikali yakiwemo majengo ya skuli mpya.

### 7.4 BODI YA SHIRIKA LA BIMA

Kamati ilipata nafasi ya kukutana na Bodi ya Shirika la Bima la Zanzibar, mnamo tarehe 9/2/2015 na kuzungumzia masuala mbali mbali yanayoonekana ni changamoto kwa Bodi hiyo na Shirika la Bima kwa ujumla.

### 7.5 CHANGAMOTO

1. Kutoongezwa kwa maslahi ya watendaji wa Shirika la Bima kulikotokana na uchelewaji wa kupata majibu kutoka Kamisheni ya Utumishi wa Umma yanayohusiana na taratibu za marekebisho ya maslahi hayo. Shirika la Bima lilitayarisha mapendekezo ya Mishahara mipya pamoja na muundo mpya wa Utumishi wa Shirika hilo (Scheme of Services) ambapo fedha kwa ajili ya utekelezaji wake tayari zimeshatengwa na Shirika. Hata hivyo, katika kufuata taratibu zinazotakiwa, Bodi ilipeleka barua Kamisheni ya Utumishi wa Umma inayohusu dhamira ya mapendekezo hayo mnamo mwezi wa Oktoba, 2014 kabla ya mapendekezo yenyewe hayajawasilishwa huko. Kamati imesikitishwa kupata taarifa kuwa barua hiyo ya mwezi Oktoba, 2014 inayohusu dhamira tu ya mapendekezo hayo imejibiwa mwezi Januari, 2015 kwa kueleza tu kuwa ombi hilo linashughulikiwa.

2. Viwango vikubwa vya fidia vinavyotozwa kwa ajili ya kulipwa mtu aliyepata athari ya kimwili kutokana na ajali (third party body injury). Kumejitokeza baadhi ya mawakili wa kujitegemea walio wajanja ambao huwafuata waathirika wa ajali kwa ajili ya kuwasimamia kesi zao mahakamani ili na wao waweza kufaidika na fidia inayotolewa kwa waathirika (walalamikaji) hao.

3. Kuchelewa kupatiwa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Shirika la Bima, Pemba. Licha ya kuwa Serikali ina majengo mengi na ardhi yote ni mali ya Serikali, suala la kupatiwa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Shirika la Bima, Pemba, limechelewa kufanyiwa kazi wakati ambapo Shirika kwa muda mrefu sasa limeshatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi hiyo. Hata hivyo, Kamati imefarajika kidogo kuona kuwa kuna mpango wa kupatiwa Shirika la Bima moja kati ya majengo ya Serikali ambalo lipo Chake Chake kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi hiyo.

4. Viwango vikubwa vinavyotozwa na Mamlaka ya Kusimamia Huduma za Bima Tanzania (TIRA). Shirika la Bima linatakiwa lilipe kiwango fulani cha fedha kwa Mamlaka ya Kusimamia Huduma za Bima Tanzania (TIRA) ambapo kwa mwaka jana 2014 lilitakiwa kulipa asilimia 20 ya mapato yake ambapo Shirika lilipa fedha zisizopungua Tsh millioni 600. Kiwango hicho cha fedha ni kikubwa na hasa ikizingatiwa kuwa hata Serikali yenyewe ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ndio

mmiliki wa Shirika hilo haikupata kiwango hicho kama mchango wa Shirika kwa Serikali. Kwa mwaka huu wa 2015 Shirika linatakiwa kulipa TIRA asilimia 10 ya fedha zote. Kiwango chote hicho kinaingia katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

5. Uanzishwaji wa Bima ya Kiislam(Takafur) katika Shirika la Bima unaonekana kukumbwa na vikwazo. Kamati ilipata taarifa kuwa Shirika la Bima limeshajiandaa kuanzisha huduma za Bima ya Kiislam (Takafur) ambapo bajeti kwa ajili ya huduma hiyo imeshatengwa. Aidha, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imetoa Kanuni za uendeshaji wa Bima hiyo ili Shirika la Bima lizipitie na wakati huo huo Mamlaka hiyo pia inasubiriwa itoe idhini ya kuendesha huduma hiyo. Hata hivyo, Kanuni hizo zilizotolewa zinalibana Shirika la Bima. Kwa mujibu wa Kanuni hizo taasisi au kampuni inayotaka kuanzisha Bima ya Kiislam inatakiwa itoe huduma hiyo tu ya Bima bila ya kujihusisha na kutoa huduma za Bima za kawaida. Hivyo, iwapo Shirika hilo linataka kuanzisha Bima ya Kiislam, linatakiwa liendeshe huduma hiyo tu ya Bima ya Kiislam pekee na liachane na kutoa huduma nyengine za Bima za kawaida. Kwa msingi huo, Kanuni hizo zinailazimisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzisha Shirika au taasisi nyengine itakatakayoweza kutoa huduma za Bima ya Kiisalm pekee.

6. Kuibuka kwa tatizo la Bima feki kunaondosha uwezo wa mashirika ya bima kuchangia katika uchumi wa Taifa.

7. Kuwepo kwa baadhi ya kampuni za bima zinazouza bima kwa bei tofauti kinyume na utaratibu.

## 7.6 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kuna haja kwa Serikali kuangalia kasoro zilizopo na kuzirekebisha ili mashirika na taasisi za Serikali zinazojiendesha wenyewe kifedha, zisiwekewe vikwazo pindi zinapotaka kuongeza maslahi ya wafanyakazi wake.
2. Viongozi wa Shirika la Bima na Bodi ya Shirikia hilo wafuatilie kwa karibu zaidi suala la upatikanaji wa jengo linalotarajiwa kupewa Shirika hilo kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Shirika hilo, Pemba.
3. Kuna haja kwa viongozi wa Shirika la Bima, na wa Bodi ya Shirika hilo pamoja na wa Wizara kukaa pamoja na viongozi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Huduma za Bima, Tanzania (TIRA) ili kujadili na kuyapatia ufumbuzi muafaka masuala mbali mbali muhimu yakiwemo ya uanzishwaji wa Bima ya Kiislam (Takafur), pamoja na viwango vya fedha vinavyotozwa na TIRA kila mwaka.
4. Shirika kwa kushirikiana na Wizara lisaidie katika kubuni njia madhubuti za kukabiliana na matatizo ya Bima feki, pamoja na utozaji wa viwango tofauti vya bei za bima kinyume na taratibu, unaofanywa na baadhi ya kampuni za bima hapa nchini.
5. Wizara, Shirika la Bima la Zanzibar kwa kushirikiana na wadau wengine wakiwemo madakatari na wanasheria wakae pamoja ili kujadiliana juu ya suala zima la utozaji wa viwango vya fidia mahakamni kwa mlalamikaji aliyepata athari ya kimwili kutokana na ajali (third party body injury)
6. Kwa kuwa baadhi ya Mashirika ya Serikali yamefanikiwa kuongeza maslahi ya wafanyakazi wake, kuna haja kwa Shirika la Bima kuchachamaa na kujizatiti ipasavyo ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi wake wanongezewa maslahi yao.

## 7.7 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

Kamati ilipata nafasi ya kupata taarifa za utekelezaji za Benki ya Watu wa Zanzibar katika tawi lake la Chake Chake (Pemba) pamoja na kukutana na Bodi ya Benki hiyo hapo Mpirani, Unguja.

## 7.8 PBZ TAWI LA CHAKE CHAKE (PEMBA)

PBZ Tawi la Chake Chake ni miongoni mwa matawi makongwe ya PBZ ambalo lilifunguliwa sambamba na uanzishwaji wa benki ya watu wa Zanzibar mnamo mwaka 1966. Huduma za kibenki zinazotolewa katika tawi hilo ni huduma za kibenki katika mfumo wa kawaida (Conventional Bank) na huduma za kibenki katika mfumo wa Kiislaam (Islamic Bank)

Hadi kufikia 31 Disemba 2014 tayari benki ya Watu wa Zanzibar, matawi ya Pemba yana jumla ya wateja 20,549 kati ya hao wateja 12,080 wamejiunga na PBZ ya kawaida na 8,469 wamejiunga na Benki ya PBZ inayofata misingi ya Shariah za Kiislam, Kwa upande wa Amana za wateja, hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2014, PBZ ilishapokea amana za Wateja zenye thamani ya billion 25.6 ikiwa billion 15.56 zimekushanywa PBZ conventional na 10.1 bilioni zimekushanywa PBZ Islamic.

Kwa upande wa mikopo, hadi kufikia 31 Disemba 2014 tayari PBZ (Pemba) imeshatoa mikopo yenye thamani ya Tsh. 16.76 bilioni kwa wateja 3,953. Aidha, kwa upande wa faida hadi kufikia 31 Disemba 2014 Benki tayari imeshakusanya faida ya Tsh bilioni 1.71 bila ya kodi; TZS, 0.60 bilioni ambazo zimekusanywa PBZ Islamic (Chake Chake) na Tsh. 1.11bilioni ambazo zimekusanywa PBZ conventional (Chake Chake).

## 7.9 CHANGAMOTO

1. **Mtandao:** Kutoa huduma nzuri katika ulimwengu wa kileo huna budi kutumia njia za kisasa ambazo watoaji wa huduma hizo kwa mfano TTCL, ZANTEL na wengineo pia wanakabiliwa na changamoto zao nyingi.
2. Kutopatikana kwa huduma za PBZ katika maeneo mbali mbali ya vijijini.

## 8.0 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kamati inaitaka PBZ kuharakisha mpango wake wa kuanzisha huduma za Benki hiyo kwa kutumia mawakala (Agency Banking) katika sehemu ambazo huduma za benki hiyo hazipatikani kwa vile huduma hiyo itapanua zaidi wigo wa huduma za Benki hiyo na kuwasaidia wananchi walio mbali na Benki hiyo hususan waishio vijijini.

## 8.1 BODI YA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

Kamati ilipata nafasi ya kukutana na Bodi ya PBZ mnamo tarehe 9/2/2015 na kuzungumzia masuala mbali mbali yanayoonekana kuwa ni changamoto kwa Benki kwa ujumla.

## 8.2 CHANGAMOTO

1. Kujitokeza kwa malalamiko miongoni mwa mameneja wa Matawi mbali mbali ya PBZ yanayotokana na baadhi ya mameneja kulipwa mishahara mikubwa zaidi ya mameneja wengine.

2. Haja ya PBZ kuongezewa mtaji na Serikali ambapo kwa upande wake Serikali bado inalitafakari suala hilo kwa kuzingatia majukumu mengi iliyonayo yanayohitaji fedha, Hata hivyo, vikao mbali mbali kati ya Wizara na PBZ kuhusiana na suala hilo vimekuwa vikiendelea.

### 8.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kwa kuwa suala la kuongezea mtaji PBZ limekuwa likijadiliwa kwa muda mrefu, kuna haja kwa PBZ pamoja na Wizara kuangalia kwa kina hoja za kitaalamu zitakazoiwezesha PBZ kufanya kazi kwa ufanisi zaidi katika mazingira ya sasa ya ushindani wa kibiashara, kitaaluma na kiteknolojia.
2. Kuna haja kwa Bodi ya PBZ kulifanyia kazi suala la tofauti ya mishahara kwa miongoni mwa mameneja wa matawi ya Benki hiyo ili kuondoa malalamiko yaliyopo ya kimaslahi na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Benki hiyo.

### 8.4 BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB)

Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) ina jukumu la kukusanya mapato ya ndani ya Serikali Kuu, Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Bodi ya Mapato, Zanzibar ilikusanya mapato yenye jumla ya Tsh 177.72 bilioni ikilinganishwa na makadirio ya Tsh 171.35 bilioni sawa na asilimia 103.72 ya makadirio. Kutokanana makusanyo hayo kuna ongezeko la kiasi cha Tsh 36.06 bilioni ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2011/12 ya Tsh 141.70 bilioni.

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Bodi ya Mapato Zanzibar inakadiriwa kukusanya Tsh. 199,700,000,000 ambapo hadi kufikia mwezi wa Januari, 2015 Bodi hiyo ilikuwa imeshakusanya jumla ya Tsh. 115,663,917,819 sawa na asilimia 57 ya makadirio.

### 8.5 CHANGAMOTO

1. Kutokuwepo kwa utamaduni wa kulipa kodi kwa hiari kwani inaonekana kuwa bado kuna baadhi ya wafanyabiashara wamejenga tabia ya kukwepa kulipa kodi (Tax Evasion).
2. Baadhi ya wafanyabiashara kutokutoa risiti katika mauzo.
3. Kutokupata idadi sahihi ya wageni wanaolala na kupatiwa huduma katika hoteli ndogo ndogo hususan zilizosajiliwa katika wigo wa kodi ya hoteli.
4. Kuwepo kwa magendo ya mafuta hapa nchini.
5. Kutokuwa na utaalamu wa kutosha kwa watendaji wa ZRB kuhusu usimamizi wa kodi katika sekta ya mawasiliano ya simu, mafuta na hoteli.
6. Kukosekana kwa jengo la Bodi ya Mapato (Pemba) linalomilikiwa na Bodi ya Mapato yenyewe.

### 8.6 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Bodi ya Mapato (ZRB) iongeze juhudu za kubuni mikakati mengine ya muda mrefu ili iweze kutekeleza vizuri zaidi mipango yake ya kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato.
2. Viongozi wa Bodi ya Mapato. Pemba wafuatilie kwa karibu zaidi katika Wizara inayohusika, suala la upatikanaji wa hati miliki ya eneo linalotarajiwa kujengwa ofisi ya Bodi hiyo kwa Pemba.
3. ZRB, ifanye jitihada za ziada za kuweza kutambua mianya ya kukwepa kulipa ili kuepusha upotevu wa fedha za Serikali zinazotokana na mapato ya kodi mbali mbali.

4. Kwa kuwa baadhi ya wawekezaji waliopewa ardhi na kuziacha hawajulikani hususan Pemba, kuna haja kwa Bodi ya Mapato (ZRB) kuwafuatilia wawekezaji hao ili kujua na kufuatilia ulipaji kodi.
5. Serikali iandae mkakati maalum utakaoweza kudhbiti ipasavyo biashara ya magendo ya mafuta hapa nchini.

## 8.7 MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA)

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeundwa kwa Sheria namba 11 ya mwaka 1995. TRA imeanza kutekeleza majukumu yake kuanzia mwezi wa Julai 1996. Kabla ya kuasisiwa TRA majukumu yanayofanywa na TRA yalikuwa yakitekelezwa moja kwa moja na Idara tatu tofauti zilizokuwa chini ya Wizara ya Fedha ambazo ni Idara ya Ushuru wa Bidhaa, Idara ya Kodi ya Mapato na Idara ya Kodi ya Mauzo. Kwa sasa TRA Zanzibar ina Idara mbili ( Idara ya Kodi za Ndani na Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa. Jukumu la Mamlaka ya Mapato (TRA) ni kukusanya mapato yatokanayo na vianzio vya Muungano ikiwemo Ushuru wa Forodha, Ushuru wa Bidhaa Kodi ya Mapato.

## 8.8 MAMLAKA YA MAPATO (TRA), OFISI YA PEMBA

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 TRA Pemba imepangiwa kukusanya Tsh 4452,664,817.63. Idara ya Forodha imepangiwa Tsh 1,020,599,567.37 na Idara ya Kodi za Ndani imepangiwa kukusanya Tsh 3,432,065,250.26.

Makadirio katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2014 ni kukusanya Shs 2,135,944,065.59 ambapo makusanyo halisi kwa TRA Pemba yalikuwa Shs 1,746,822,099.68 ambazo ni sawa na 82%.

## 8.9 CHANGAMOTO

1. Kiwango kidogo cha uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi.Wafanyabiashara wengi wa kisiwa cha Pemba wanaoingiza bidhaa wanatumia bandari ya Unguja kuingiza bidhaa zao zinazotoka nje ya nchi.
2. Biashara ya magendo ya Mafuta inayofanyika baharini na nchi kavu inapunguza mapato ya Taasisi za Kodi kisiwani Pemba.
3. Kiwango kidogo cha Elimu kwa baadhi ya wafanyabiashara kisiwani Pemba kinakuwa kikwazo katika ulipaji wa kodi kwa hiari.
4. Miundombinu ya Bandari za Pemba haikidhi mahitajio ya soko la wafanyabiashara. Hakuna vifaa muhimu vinavyoruhusu meli kubwa za mizigo kushusha mizigo ya wafanyabiashara kutoka nje ya nchi.

1. Wafanyabiashara wengi waliopo kisiwani Pemba ni wadogo (SME’s).

## 9.0 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Pamoja na kuwa programu ya elimu ya kodi hufanywa kila baada ya miezi mitatu, kuna haja kwa TRA kufanya mpango wa kuongeza idadi ya wafanyakazi hususan wa kuelimisha masuala ya kodi kwa kuwa kitengo cha elimu kwa walipakodi cha TRA kina wafanyakazi wachache sana ambapo kwa Unguja kina wafanyakazi wawili tu na Pemba hakuna mtoa elimu ya kodi.

2. Kwa kuwa kuna uelewa mdogo juu ya Jumuiya ya Forodha ya Afrika ya Mashariki na faida zake, kuna haja kwa Serikali kuangalia namna Zanzibar itakavyofaidika na Jumuiya hiyo na kusambaza elimu hiyo kwa wadau mbali mbali.

3. TRA izidishe kasi ya utoaji elimu wa masuala ya ulipaji kodi hususan vijijini ili kuwafanya wananchi waweze kulipa kodi kwa hiari.

4. Kuna haja kwa TRA kutoa elimu maalum juu ya kodi ya zuio ili kuepusha migongano baina ya TRA na kampuni mbali mbali hususan kampuni za mafuta.

## 9.1 MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA) - OFISI YA ZANZIBAR

Katika mwaka wa Fedha 2014/2015 Ofisi ya Zanzibar ya Mamlaka ya Mapato Tanzania imepangiwa lengo la kukusanya Tsh 166,056 millioni. Lengo hilo limeongezeka kwa zaidi ya asilimia 21.5 ikilinganishwa na mapato halisi yaliyokusanywa katika mwaka wa Fedha wa 2013/2014 ambapo TRA ilikusanya Tsh 136,690.8 millioni.

Katika kipindi cha Julai - Disemba, 2014, Ofisi ya Zanzibar ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ilipangiwa kukusanya Tsh 81,965.9 millioni kutoka Idara zote mbili (Idara ya Kodi za Ndani na Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa). Mapato halisi kwa kipindi hicho ni Tsh 70,394.4 millioni sawa na asilimia 86 ya makadirio ya kipindi hicho na asilimia 42 kwa lengo la mwaka.

Aidha, kwa upande wa misamaha ya kodi, kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2014 jumla ya kodi ya Tsh 11,185.2 millioni imesamehewa kwa wadau mbali mbali. Asilimia 60 ya msamaha huo umetumiwa na Wawekezaji waliosajiliwa na ZIPA. asilimia 14 umetumika kwa Mashirika ya Umma, asilimia 11 umetumika kwa taasisi za Serikali, asilimia 8 imetumika kwa Washirika wa Maendeleo waliosaidia Serikali katika miradi mbali mbali, asilimia 6 imetumika kwa watu binafsi na asilimia 1 kwa taasisi za Dini.

## 9.2 CHANGAMOTO

i. Muundo wa TRA Zanzibar unaonesha kuwa TRA Zanzibar inaongozwa na Naibu Kamishna ambae anawajibika moja kwa moja kwa Kamishna wa Forodha. Hali hii inaonesha kuwa Naibu Kamishna wa TRA Zanzibar yupo katika ngazi ya nne katika mtiririko wa ngazi za uongozi wa TRA ambazo ni Kamishna Mkuu wa TRA, Naibu Kamshna Mkuu wa TRA, Makamishna wa TRA, Naibu Kamishna wa TRA.

ii. Katika miaka ya hivi karibuni kumejitokeza tofauti kubwa ya bei za bidhaa kati ya Unguja na Pemba ambapo bidhaa zinaonekana kuuzwa kwa bei kubwa zaidi kisiwani Pemba.

## 9.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ishirikiane na TRA (Makao Makuu) ili kasoro iliyopo ya kumfanya Naibu Kamishna wa TRA Zanzibar kuwa katika ngazi ya nne katika ngazi za uongozi wa TRA anaewajibika kwa Kamishna wa Forodha iweze kurekebishwa.

2. Kamati inaishauri TRA kwa upande wake kuliangalia kwa makini na kulichukulia hatua suala lililojitokeza hivi karibuni la ughali mkubwa wa bei za bidhaa zinzouzwa Pemba ikilinganishwa na Unguja.

3. Kuna haja kwa TRA kuandaa mkutano wa pamoja utaowashirikisha watendaji wa Bodi ya Mapato (ZRB), Jumuiya ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima (ZNCCIA), Shirika la Bandari pamoja na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo utaojadili masuala mbali mbali muhimu yakiwemo ya kodi, misamaha ya kodi, na bandari bubu.

4. Kwa kuwa hivi sasa baadhi ya wafanyabiashara wa Pemba hushusha bidhaa zao katika bandari ya Mombasa, kuna haja kwa Serikali kuchukua juhudi za makusudi zitakazowashawishi wafanyabiashara hao kushusha bidhaa zao Pemba na kuongeza mapato ya Serikali kupitia kodi mbali mbali.

## 9.4 BENKI KUU YA TANZANIA (BOT) TAWI LA ZANZIBAR

Jukumu la Benki Kuu (BOT) Tawi la Zanzibar ni kutekeleza kazi za Benki Kuu kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Benki Kuu ya Mwaka 2006 ambazo ni kuwa Benki ya Serikali, Benki ya Mabenki na Mshauri wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mapato na matumizi (fiscal policy) pamoja sera za uchumi.

Katika kipindi cha Julai – Disemba, 2014, Tawi lilitekeleza kazi mbali mbali zikiwemo kuhifadhi fedha za Serikali na Mabenki, Kutoa ushauri kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar,, kushiriki katika vikao vya Serikali, kuboresha takwimu katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, uandaaji wa taarifa za uchumi na usambazaji wa majarida ya uchumi, kufanya tafiti za kiuchumi ikiwemo utafiti juu ya zao la karafuu na utafiti juu ya Sekta ya utalii.

**Kwa mujibu wa BOT, zimebainika changamoto mbali mbali zinzoukabili uchumi wa Zanzibar kama ifuatavyo:**

1. Uchache wa makusanyo ya Kodi za Ndani katika hoteli za kitalii. Makusanyo ya kodi za ndani bado ni madogo ikilinganishwa na mahitaji ya msingi hasa matumizi kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Idadi kubwa ya uingiaji wa watalii pamoja na ukuaji wa uchumi kwa ujumla hauiendi sambamba na ukuaji wa makusanyo ya kodi hasa kutoka katika hoteli za kitalii. Hivyo, Serikali inashauriwa kupanua wigo wa kodi na kubuni mikakati ya kutoza kodi inayostahiki hasa kwa Sekta ya Utalii.

2. Sekta ya uvuvi ni muhimu lakini mchango wake bado ni mdogo. Takwimu zinaonesha kuwa kwamba sekta ya uvuvi unachangia wastani wa asilimia 1.3 tu ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi, licha ya kuanzishwa Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu (Deep Sea Fishing). Hivyo, kuna haja ya kuwa na mikakati ya muda mfupi na mrefu ya kuwasaidia wavuvi wadogo. Vile vile Mamlaka ya Ukuzaji, Vitega Uchumi (ZIPA) iwavutie wawekezaji katika uvuvi hasa maeneo ya bahari kuu na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kusindika samaki.

## 9.5 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri BOT kufanya utafiti wa kina juu ya namna ya idadi ya watalii wanaoingia Zanzibar wanavyoweza kukuza zaidi pato la Taifa pamoja na kufanya utafiti ili kujua namna ya "Package Tourism" unavyoathiri au kumufaisha uchumi wa Zanzibar.
2. Kwa kuwa mapato ya ndani bado ni kidogo, Kamati inaishauri BOT kuongeza juhudi za kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya namna bora zaidi ya kuimarisha mapato ya ndani na kuinua uchumi wa Taifa kwa ujumla.

3. Kamati inaishauri BOT kuhamasisha wawekezaji kuanzisha Benki ya Wakulima au kuruhusu Benki zilizopo kufungua huduma za Benki ya wakulima ili Benki hizo ziweze kuwahudumia wakulima kwa ufanisi zaidi.

4. Kwa kuwa BOT inashughulikia masuala mbali mbali ya utafiti ikiwemo utafiti wa zao la karafuu, Kamati inaiomba BOT kukisaidia kifedha na kitaaluma kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Matangatuani ambacho tayari kimashaanza kufanya utafiti wa miche ya mikarafuu.

**9.6 MFUKO WA WA HIFADHI YA JAMII (ZSSF)**

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) umeanzishwa chini ya Sheria namba 2 ya mwaka 1998 na kufanyiwa mapitio na kuundwa upya kwa Sheria namba 2 ya mwaka 2005. Lengo la Mfuko huu ni kuwa na utaratibu endelevu wa kulipa mafao ya uzeeni kama sehemu ya hifadhi ya jamii. Lengo hili linatimizwa kwa kusajili wanachama, kukusanya michango yao, kuwekeza fedha hizo katika miradi yenye tija na hatimae kutoa mafao kwa wanachama muda unapofika. Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Mfuko wa hifadhi ya Jamii, Zanzibar na katika ofisi yake ya Pemba, pamoja na Viwanja vya Kufurahishia Watoto vya Kariakoo na Tibirinzi katika vipindi tofauti.

**9.7 CHANGAMOTO**

1. Matokeo ya udanganyifu kwa baadhi ya waajiriwa wa Serikali hali ambayo hupelekea fedha za Mfuko huo kupotea.

2. Kutokuwa na Hati Miliki ya kiwanja cha Mwanakwerekwe.

3. Udhibiti wa mapato kulingana na idadi ya wanaoingia katika kiwanja cha Kariakoo.

4. Uhaba wa wafanyakazi katika Idara ya Usimamizi wa Ujenzi.

**9.8 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri ZSSF kuwasaidia sana wazee na wastaafu wenye ulemavu kwa kuwapatia mafao yanayostahiki.
2. Kamati inaishauri ZSSF kuongeza wafanyakazi hususan kwa upande wa Usimamizi wa Ujenzi, kwa sababu Ofisi nzima ina mfanyakazi mmoja tu mwenye kuhusiana na fani hiyo.

## 9.9 OFISI YA ZSSF, PEMBA

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Pemba unatekeleza majukumu yake kwa mashirikiano na Afisa Mdhamin wa Wizara ya Fedha pamoja na watendaji wa Ofisi hiyo.

## 10.0 CHANGAMOTO

1. Ugumu wa kuwasajili wafanyabiashara wadogo wadogo ambao kundi kubwa liko katika Sekta isiyo rasmi
2. Madai ya marejesho ya michango kwa wafanyakazi wa sekta binafsi ambao ajira zao ni za mikataba ya muda mfupi. Aidha, madai hayo pia hutokea kwa wafanyakazi wa taasisi za Serikali wanaoachishwa au kufukuzwa kazi kabla ya umri wa kustaafu.
3. Masuala ya kiutumishi hasa kumbukumbu za wanachama wa Mfuko kwa baadhi ya wakati zinatofautiana baina ya Mfuko na taasisi wanazofanyia kazi.
4. Kutokuwepo kwa taasisi kwa taasisi mpya za binafsi.

## 10.1 MFUKO WA BARABARA ZANZIBAR

Kwa ujumla majukumu ya msingi ya Mfuko wa Barabara ni kuhakikisha kuwa fedha za matengenezo ya barabara zinakusanywa na vyombo vilivyowekwa na kuwasilishwa katika Mfuko wa Barabara. Aidha, Mfuko wa Barabara una jukumu la kuhakikisha matumzi mazuri ya fedha hizo na kuwepo ukaguzi wa mara kwa mara na ule wa kila mwaka. Mfuko wa Barabara hutunza fedha na kuajiri watengenezaji wa barabara. Mfuko huwa ni mdhibiti wa fedha na kusimamaia ujenzi wa barabara ili kuhakikisha kuwa malengo ya mwaka yanafikiwa na viwango vinapewa kipaumbele.

## 10.2 CHANGAMOTO

1. Sheria inayotumika kuwa imeshapitwa na wakati.
2. Uchakavu wa vifaa vya kujengea barabara.
3. Uhaba wa wafanyakazi.

## 10.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Mfuko wa Barabara kuwa na Mshauri ndani Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu ili kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi zao.
2. Kamati inaomba Serikali pamoja na Wizara husika kuifanyia marekebisho Sheria ya Mfuko wa barabara ambayo inatumika. Hivyo Sheria hiyo irekebishwe ili kuwepo kwa ushirikishwaji wa kutosha kwa Mfuko wa Barabara hususan katika ingiliaji wa mikataba pamoja na utekelezaji wa kazi utengenezaji wa barabara.
3. Kamati inashauri Wizara ya Fedha kuingiza Fedha kwa wakati. Ili mategenezo ya barabara yaweze kufanyika bila ya kuchelewa kwa vile kuchelewa kuzitengeneza barabara hizo kunapelekea usumbufu mkubwa kwa watumiaji na ajali za mara kwa mara za barabarani.

## 10.4 CHUO CHA UONGOZI WA FEDHA, CHWAKA

Chuo cha Uongozi wa Fedha ni Chuo kinachotoa mafunzo ya ngazi ya cheti, stashahada na shahada katika fani ya Uhasibu, Fedha, Benki Manunuzi, Ugavi na TEHAMA.

**10.5 CHANGAMOTO**

1. Ukosefu wa maji safi na salama katika Chuo hicho.
2. Kutoshirikishwa kwa Uongozi wa Chuo cha Uongozi wa Fedha katika mchakato wa kukihamisha Chuo hicho kuwa katika Usimamizi wa Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).
3. Tangazo la Gazeti la tarehe 21/07/2014 kuhusiana na kauli iliyotolewa na NECTA ya kuwa miongoni mwa Vyuo 66 Vya Tanzania vinavyotakwa kufutwa kimoja wapo ni Chuo Cha Usimamizi wa Fedha Chwaka.
4. Uhaba wa madarasa pamoja na Ofisi za walimu ndani ya Chuo hicho.
5. Uongozi wa Chuo kutoshirikishwa katika mchakato mzima wa utungaji wa Sheria.
6. Kutoingiziwa fedha kwa wakati (budget) ya mwaka hali ambayo inapelekea Chuo kupata usumbufu wa kiutendaji katika Chuo hicho.

**10.6 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.**

1. Kamati inaiomba Serikali na Wizara husika kutokihamisha Chuo hiki kwenda katika Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Ili kuweza kukipa uwezo Chuo hicho kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

2. Kamati inaishauri Uongozi wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Chwaka kujipanga vizuri wakati wa Sheria inayohusu marekebisho ya Chuo hicho kupitishwa.

**10.7 MAMLAKA YA UKUZAJI VITEGA UCHUMI (ZIPA)**

Jukumu kubwa la Mamlaka hii ni kuwashajiisha wawekezaji wa nje na ndani kuwekeza nchini pamoja na kuwasaidia wawekezaji kufikia malengo ya uwekezaji.

**10.8 CHANGAMOTO**

Uvamizi katika baadhi ya maeneo huru ya Uwekezaji, Fumba unaofanywa na wananchi kwa shughuli za ujenzi wa nyumba za kuishi.

**10.9 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kuna haja kwa mamlaka kuzidisha utoaji wa elimu kwa wananchi, viongozi na wawekezaji mbali mbali juu ya taratibu za Serikali katika ardhi ya wawekezaji.

2. Mamlaka iharakishe juhudi zake za kukamilisha miundombinu mbali mbali katika maeneo huru ya uwekezaji ikiwemo miundombinu ya barabara.

## SEHEMU YA NNE
## WIZARA YA BIASHARA VIWANDA NA MASOKO

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imeundwa na Idara nne na Mashirika mawili pamoja na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:-

1. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
2. Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko.
3. Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiriamali.

4. Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
5. Afisi Kuu – Pemba.
6. Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC).
7. Shirika la Biashara ya Magari.

## 11.0 MAPATO NA MATUMIZI

Katika kikao cha kujadili taarifa ya utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara, Kamati iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara iliweka lengo la kukusanya ya Tsh 100.0 millioni kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali. Kwa kipindi cha Julai – November, Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Tsh 19,571,682 milioni kutoka katika vianzio vyake vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 November, 2014 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Tsh 22,197,500 milioni na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Aidha, Kamati ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imetengewa Tsh 5,864.30 millioni kwa ajili ya kutekeleza malengo iliyojiwekea. Kati ya fedha hizo Tsh 2,486.3 millioni ni kwa kazi za kawaida na Tsh 2,335.7 kwa kazi za maendeleo na Tsh 1,042.3 millioni kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi za Wizara. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2014 Wizara ilikwishaingiziwa jumla ya Tsh 1,534.94 millioni sawa na asilimia 49.5% ya bajeti ya mwaka na asilimia 26.2% ya fedha zilizoombwa.

## 11.1 IDARA YA BIASHARA NA UKUZAJI MASOKO

Jukumu kubwa la Idara hii ni kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za biashara pamoja na kuzitafutia masoko endelevu ndani na nje bidhaa zinazozalishwa nchini na kuitangaza Zanzibar katika masoko ya ndani na nje.

## 11.2 CHANGAMOTO

1. Bado kuna baadhi ya wafanyakazi wadogo wadogo wanuingiza biashara zilizopigwa marufuku uingizwaji wake nchini kwa mujibu wa Sheria ya Biashara na Leseni ya Zanzibar ya mwaka 2013.

2. Katika kudhibiti matumizi ya bidhaa zisizofaa kwa mujibu wa Sheria ya Biashara ya mwaka 2013, bidhaa nyingi hukamatwa ila changamoto iliyokuwepo ni gharama za kuziangamiza bidhaa hizo (zisizo za vyakula) bali gharama za kuangamiza bidhaa za vyakula hutoa wafanyabiashara wenyewe.

## 11.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kwa kuwa kumejitokeza tofauti kubwa katika bei za bidhaa kwa upande wa kisiwa cha Pemba na Unguja katika miaka ya hivi karibuni. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuwa waangalifu zaidi katika kulitatua tatizo hilo linalowakumba wafanyabiashara wetu wadogo wadogo.

2. Kamati inaihimiza Wizara kuharakisha uandaji wa Sheria ya wafanyabiashara wadogo wadogo ili kuweza kuweka mazingira mazuri zaidi katika uendeshaji ya biashara hiyo.

## 11.4 IDARA YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UKUZAJI UJASIRIAMALI

Jukumu kubwa la Idara hii ni kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya ukuzaji ujasiriamali pamoja na kusimamia kazi za Kituo cha Maendeleo ya Viwanda.

Aidha, mnamo tarehe 13/02/2015 Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi ilipata fursa ya kukutana na kupokea tarifa ya Jumuiya ya wajasiriamali wa "UWAMWIMA" iliopo mkunazini ambapo changamoto kadhaa zinazoikabili Jumuiya hiyo pamoja na wajasiriamali wengine kwa ujumla zilijadiliwa.

## 11.5 CHANGAMOTO

1. Mahoteli kukataa kusaini mikataba na wakulima wadogo wadogo wanaosambaza mazao yao mahoteli. Kutokana na halii hii wajasiriamali kuendelea kupoteza haki zao za msingi za kimaisha na kuendelea na kuwa na hali duni za kimaisha.

2. Uhaba wa eneo la Ofisi kutokana na matumizi na mahtaji walionayo hayakidhi mahitaji.

3. Ukosefu wa soko la kudumu la kuuzia mazao.

4. Mahitaji makubwa ya mikopo kwa wajasiriamali wadogo wadogo hususan katika mabenki hali ambayo hurudisha nyuma maendeleo ya wajariamali hao.

5. Ukosefu wa mitaji kwa wajasiriamali.

## 11.6 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba jumuiya ya "UWAMWIMA" kuajiri wataalamu hususan katika idara ya masoko kwa pande zote mbili kwa Unguja na Pemba.

2. Kamati inaishauri jumuiya ya "UWAMWIMA" kutoa elimu juu ya umuhimu wa upandishaji na utumiaji wa mboga mboga katika taasisi pamoja na vikundi mbali mbali vya wakulima ili kuweza kulinda na kutunza afya zetu pamoja na vizazi vyetu vijavyo.

## 11.7 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika limepanga pamoja na utekelezaji wa mpango wake wa mageuzi, kuendelea na utekelezaji wa shughuli zake za kawaida kama vile kufanya ununuzi wa karafuu, kuajiari wafanyakazi kumi na tatu (13) wapya, kujenga vituo saba (7) vya ununuzi wa karafuu, ununuzi wa mezani 30 za kisasa, ununuzi wa mitambo na ujenzi wa uzio wa kiwanda cha Makonyo, kufanya utafiti wa karafuu ya Zanzibar ili kubainisha vigezo vya upekee, uanzishaji wa kiwanda kidogo cha majaribio cha uzalishaji wa mafuta ya mimea na mengineyo.

## 11.8 CHANGAMOTO

1. Pamoja na kupungua Biashara ya magendo ya Karafuu bado Biashara hiyo inaendelea kuwa ni changamoto kwa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) hususan katika njia za vizibiti (Road Blocks) za barabara. Aidha, kwa upande wa baharini doria zinazofanywa kutokidhi haja kikamilifu kutokana na ufinyu wa Bajeti inayoingizwa kwa ajili ya kazi hizo.
2. Kamati ilielezwa pia kuwa kulijitokeza tatizo la ubadilishanaji wa karafuu kwa bidhaa yengine unaofanywa na wakulima na wafanyabiashara wengine.
3. Kujitokeza tatizo la baadhi ya wanavijiji kununua karafuu kwa jina la Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC), hali ambayo hupelekea soko la karafuu kupungua katika Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

4. Ukosefu wa elimu kwa wakulima wa karafuu juu ya muhimu wa uhifadhi wa karafuu wakati wa upandishaji, uvunaji pamoja na hatua za uanikaji. Kutokana na hali hii kupelekea viwango vya karafuu kushuka kwa kiasi kikubwa.

## 11.9 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kuwa waangalifu zaidi katika soko la karafuu hususan katika biashara ya magendo.

2. Kamati inaitaka Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kuliangalia vizuri na kulichukulia hatua zifaazo suala la ubadilishanaji wa karafuu na bidhaa nyengine unaofanywa na baadhi ya wakulima wa Karafuu na wafanyabiashara.

3. Kamati inaishauri Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kuendelea kutoa elimu kwa wakulima wadogo wadogo juu ya umuhimu wa uzalishaji wa zao karafuu kupitia katika vyombo ya habari.

4. Kamati inaiomba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kupitia Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kukaa pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Matangatuani ili kulichukulia hatua zinastahiki zoezi la tafiti ya miche ya mikarafuu.

## 12.0 OFISI YA ZSTC – DUBAI

Kamati ilipata taarifa ya kuhusu mageuzi ya Shirika ambapo hatua mbali mbali zilichukuliwa katika mageuzi hayo zikiwemo kufanya tafiti za mapitio ya sekta ya karafuu, uendeshaji wa biashara ya karafuu, kuuza bidhaa nyengine zinazozalishwa na Shirika kupitia kiwanda cha Makonyo na mfumo unaotumika kwa uendeshaji wa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) lililopo Dubai. Jitihada hizi zinaendelea kufanywa kwa lengo la kutanua soko la karafuu katika nchi zinazopakana na Falme za Kiarabu, kwa kutumia Kituo cha Dubai kuonekana faida itapatikana sio kwa karafuu tu hata kuitangaza Zanzibar baada ya Mradi wa "Branding" kukamilika.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Tawi la Dubai lilikusanya faida ya Tsh 333,47.0 milioni na jumla ya Tsh 561.2 milioni zilitumika wakati makadirio ilikuwa kutumia Tsh

534.0 milioni. Matumizi yamezidi makadirio kutokana na kuongezeka kwa karafuu zilizowasilishwa Tawini.

**12.1 CHANGAMOTO**

Usafirishaji wa karafuu kwa njia ya magendo kupelekwa nchi jirani hali ambayo kupelekea kuzorota kwa shughuli za Shirika kwa ujumla na kushindwa kutoa mgao wa karafuu kwa Tawi la Dubai.

**12.2 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

Kamati inaishauri Wizara kupitia Shirika la Biashara la Taifa la Zanzibar (ZSTC) kuendelea kutoa elimu juu ya upandaji wa mikarafuu kwa wingi kwa wakulima wetu wa Unguja na Pemba ili kuweza kukabiliana na hali ushindani katika soko la dunia.

**12.3 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS)**

Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Viwango Na. 1 ya Zanzibar ya mwaka 2011. Taasisi hii imeanza kazi zake rasmi September,2012. Majukumu makuu ya Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) ni kuweka viwango na kusimamia ubora wa bidhaa na huduma nchini, iwe zinazozalishwa au kuingizwa nchini kutoka nje ya nchi na kuimarisha biashara katika soko la ndani pamoja na biashara za kimataifa. Hali hiyo inatarajiwa kuwa ni chachu ya maendeleo, kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umasikini pamoja na kulinda afya na usalama kwa watumiaji wa bidhaa na huduma pamoja na kuhifadhi mazingira ya nchi yetu.
Katika kipindi cha Julai - November 2014, Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) imetekeleza majukumu yake kama ilivyojipangia kupitia malengo makuu ya utekelezaji kama yalivyo katika mpango mkakati na mpango kazi wa kipindi hicho. Utekelezaji huo umehusisha kuandaa viwango 80 vya bidhaa pamoja na kuendelea na hatua za ajira kwa wafanyakazi 22 wapya

**12.4 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Taasisi ya Viwango (ZBS) ni Taasisi inayohitaji fedha nyingi ii kuakamilisha ipasavyo malengo yake, hivyo kuna haja kwa Serikali kuongeza kasi ya uingizaji wa fedha kwa Taasisi hii ili iweze kuongeza kasi ya ufanisi katika utendaji wake.

2. Kwa kuwa Taasisi bado ni changa, ipo haja kwa viongozi wa Taasisi kukuza ushirikiano na Taasisi kama hizo ikiwemo TBS (Tanzania Bara) pamoja na nyengine za nchi jirani.

**SEHEMU YA TANO**

**12.5 HITIMISHO**

Kwa ujumla Kamati imefanikisha majukumu yake ya kufuatilia utekelezaji wa kazi katika Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara hizo zilizoainishwa katika ripoti hii. Kamati inazipongeza Wizara na taasisi hizo kwa juhudi zinazochukua katika utekelezaji wa kazi zao.

Kamati pia inapenda kutoa shukurani kwa wale wote waliofanikisha kazi za Kamati kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na pia kuwezesha taarifa za Kamati kutayarishwa na kuwasilishwa kunakohusika. Kamati inawashukuru kwa dhati viongozi na watendaji wote wa Serikali na wa Baraza pamoja na wale wote waliofanikisha kazi za Kamati.